

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S.L.P 02,  
**USHIROMBO**  
BUKOMBE

**MKOA WA GEITA:**  
**Simu:** 028 2520709  
ded@bukombedc.go.tz

15/05/2017



Kumb. Na. F.20/26/126.

**TANGAZO! TANGAZO!**

**KWA WANANCHI WOTE,  
TANZANIA.**

**YAH: LGA/113/2016/2017/PQ/ TANGAZO LA ZABUNI MBALIMBALI  
KWA  
MWAKA WA FEDHA 2017/2018.**

Halmashauri ya wilaya ya Bukombe inakaribisha maombi ya Zabuni kutoka taasisi/ Kampuni/Vikundi/Watu binafsi wenye leseni na uwezo wa kutoa huduma zinazotakiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kwa kipindi cha kuanzia **Julai 2017 – Juni 2018**, kama ifuatavyo:

- 1.LGA 113/2016/2017/PQ /1:ZABUNI YA KUTOA VIFAA VYA MAABARAHOSPITALI YA WILAYA.**
- 2. LGA 113/2016/2017/PQ/2: ZABUNI YA KUTOA HUDUMA (INSTALLATION) ZA UMEME NA SOLAR.**
- 3. LGA 113/2016/2017/PQ./4: ZABUNI YA UJENZI WA MAJEGO NA BARABARA(WORKS CONSTRUCTION).**
- 4. LGA 113/2016/2017/PQ /5.: ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA UCHAPISHAJI NYARAKA ZA HALMASHAURI.**

**5. LGA 113/2016/2017/PQ /6 : ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA UUZAJI WA MADAWAYA BINADAMU.**

**6. LGA 113/2016/2017/PQ/7: ZABUNI YA UCHAPISHAJI NYARAKA MBALIMBALI ZA HALMASHAURI.**

**7. LGA 113/2016/2017/PQ /8: ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA MGAHAWA HALMASHAURI (HQ).**

**8. LGA 113/2016/2017/PQ /9: ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA MGAHAWA HOSPITALI.(W).**

**9. LGA 113/2016/2017/PQ /10 : ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA ULINZI HOSPITALI YA WILAYA.**

**10. LGA 113/2016/2017/PQ /11. ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA ULINZI HALMASHAURI YA WILAYA.**

#### **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA ZABUNI**

4. Mwombaji awe amesajiliwa na kuwa na namba ya TIN na Leseni hai
5. Mwombaji anatakiwa kuambatanisha picha ndogo (Passport size) kwenye barua ya maombi yake.
6. Mwombaji wa shuguri za ujenzi aonyeshe CRB hai ya kampuni yake,Daraja lake, Leseni hai na wataalamu alionao.

**Kwa upande wa uuzaji wa madawa na vifaa vya maabara mwombaji awe na sifa zifuatazo:-**

**Mwombaji wa vifaa vya maabara, Vifaa Tiba na madawa awe na kibali kilicho tolewa na wizara ya Afya.**

**KWA MADAWA;**

- Orodhesha aina ya vifaa ulivyonavyo na bei
- Iwe Pharmacy iliyosajiliwa na Bodi ya chakula na madawa(TFDA)
- Iwe na mfamasia aliyeajiliwa na Pharmacy Council.
- Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vielelezo.
- Awe na kibali kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Vifaa vya Maabara)

7. Mwombaji ataje bei zake kwa kipimo cha huduma .
8. Mwombaji anaweza kuomba zabuni zaidi ya moja kwa kuzingatia kipengele cha masharti haya, lakini kila **ZABUNI** iwe na nakala halisi ya stakabadhi ya ada na barua ya peke yake.
9. Ada ya maombi ni **Tsh. 100,000/=** ambazo *hazitarudishwa*. **Malipo yote yalipwe kupitia Account No. 32510000704 NMB tawi la Bukombe na kisha kuleta Nakala ya malipo ya Benki (Pay in Slip) Ofisi ya Fedha ili kukatiwa stakabadhi ya Halmashauri.**
10. Maombi ya zabuni yaandikwe kwa herufi kubwa yakionyesha aina ya zabuni na jina la zabuni inayohusika na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wowote yafungwe kwa **lakiri** na yatumwe na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni lililoko kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kwa anuani iliyo hapo chini;

**Mkurugenzi Mtendaji (W)**  
**S.L.P 2,**  
**BUKOMBE**

11. Maombi yote yatumwe na kutumbukizwa kwenye saduku la zabuni lililoko katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) saa za kazi kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri.
12. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15/06/2017** saa 4:00 asubuhi. Ikifuatiwa na zoezi la kufungua zabuni litakalo fanyika saa 4:30 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe mbele ya wazabuni wote au wawakilishi wao watakao hudhuria.
13. Waombaji wote wanakaribishwa au wawakilishi wao kuwepo siku ya ufunguzi tarehe **15/06/2017**.
14. Maombi yote ya zabuni yatakayochelewa na yale ambayo hayatafunguliwa wala kusomwa hadharani mbele ya wazabuni au wawakilishi wao hayatapokelewa wala kufanyiwa tathmini.
15. **KWA ZABUNI YA ULINZI MWOMBABI LAZIMA AELEZE KIASI CHA GHARAMA ZA MALIPO KWA KUTUMIA SILAHA,NA KWA VIRUNGU.**

- ***KWA ZABUNI AMBAZO UTEUZI WAKE UKO CHINI YA GPSA NA TEMESA MKOA WA GEITA TU ( TEMESA KWA MAGARI NA MITAMBO) MZABUNI ALIYE TEULIWA,ALETE UTEUZI WAKE HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE OFISI YA MANUNUZI.***

Wenu katika Ujenzi wa Taifa.

Dionis Myinga,  
MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
**BUKOMBE.**

**Nakala:**

PPRA,  
**DAR ES SALAAM.**

KATIBU TAWALA (M),  
**GEITA**

KATIBU TAWALA (W),  
**BUKOMBE.**

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya:-

**Mbogwe, Shinyanga (V), Meatu, Bariadi, Kishapu, Maswa, Kahama, Geita, Kibondo, Biharamuro,Ngara, na Chato.**

Mbao zote za matangazo (W)  
**BUKOMBE.**